



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA UMMA

**KUFUNGULIWA KWA OFISI MPYA ZA LATRA-TEGETA, KAHAMA,
MAKAMBAKO, NA KUHAMISHWA KWA OFISI ZA MIKOA YA
MARA, KATAVI, NA SIMIYU.**

Dar es Salaam,

Tarehe 3 Oktoba, 2023.

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inawataarifu wananchi na wadau wote wa usafirishaji kuwa imefungua ofisi mpya za LATRA katika Wilaya zifuatazo;

KINONDONI- Eneo la Tegeta katika jengo la **Kibo Complex** sakafu ya chini ilipokuwa ofisi ya TTCL zamani.

MAKAMBAKO- Jengo la ofisi za **Tazara** karibu na mzunguko wa barabara ya Mbeya/ Njombe, na

KAHAMA- Jengo la **Mafao NSSF** ghorofa ya tatu.

Aidha Mamlaka imehamisha ofisi ya Mkoa wa Mara ,Katavi na Simiyu kutoka katika majengo ya awali na kwenda katika majengo yafuatayo;

MARA- Mtaa wa Gandhi/Mukendo Jengo la **NHC** ghorofa ya pili.

KATAVI- Mpanda Plaza jengo la **NHC** ghorofa ya kwanza, na

SIMIYU- Wilaya ya Bariadi eneo la Malambo, Barabara ya PSPF nyumba namba 12.

Hivyo, Mamlaka inawakaribisha wananchi na wadau wote wa usafirishaji katika ofisi zetu ili kupata huduma za usafiri ardhini.

**Imetolewa na;
Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**